

MARUDIO YA KISWAHILI DARASA LA TANO.

MADA: MAAMKIZI

Andika jibu la maamkizi haya.

1. Habari? - _____
2. Uhali gani? - _____
3. Waambaje? _____
4. Sababkheri? - _____
5. Masababkheri? - _____
6. Alamsiki? - _____
7. Shikamoo- _____
8. Chewa?- _____
9. Salaam aleikum - _____
10. Buheri - _____
11. Buriani - _____
12. Hujambo? - _____
13. Umeshindaje? - _____
14. Umeamkaje? - _____

MADA: NGELI

11. Tunga sentensi tano katika ngeli hizi katika hali ya umoja na wingi.

A-WA: Mfano: Paka anakunywa maziwa-paka wanakunywa maziwa

- a) _____
- b) _____
- c) _____
- d) _____
- e) _____

LI-YA.

- a) _____
- b) _____
- c) _____
- d) _____
- e) _____

KI-VI

- a) _____
- b) _____
- c) _____
- d) _____
- e) _____

I-ZI

- a) _____
- b) _____
- c) _____
- d) _____
- e) _____

Vivumishi vya sifa.

Jaza jedwali lifuatalo ukitumia kiambishi ulichopewa. Jaza katika hali ya umoja na wingi.

Zingatia ngeli.

NGELI/KIAMBISHI	SIFA					
	-embamba	-baya	-ekundu	-zito	safi	ghali
A-WA	Mwembamba Wembamba					
KI-VI						
U-I						
I-ZI						
YA-YA						
LI-YA						
U-U						




MSAMIATI WA SEBULENI.

Tumia majina yaliyo kwa jedwali kujaza pengo kwenye picha.

Kochi Runinga Takia Kinanda Meza Redio Rafu Dari Sofa,picha, shubaka, meza, kiti



Tambua msamiati huu wa porini.







Chagua jibu sahihi kujaza nafasi zilizo wazi.

Mzee Tembo aliingia. _____ daladala. Akateua kiti 2. _____ pembezoni huko nyuma 3. _____ gari hili maridadi 4. _____ Thika. Kabla hajaivuta pumzi 5. _____ kubwaga moyo, abiria wengine 6. _____ wakaingia garini na kuketi 7. _____ viti vile 8. _____ nyuma alikokaa Mzee Tumbo. Hapo nyuma 9. _____ . Wakawa abiria watatu nyuma . Naam, 10. _____ ndivyo yalivyo madaladala 11. _____ kwenda Thika; mji 12. _____ upande 13. _____ Kaskazini Mashariki mwa 14. _____ la Nairobi. Abiria 15. _____ wawili waliketi na Mzee Tumbo.

A	B	C	D
1. katika	katikati	kwenye	mwake
2. cha	wa	za	ya
3. cha	wa	za	ya
4. iendalo	liendalo	kiendacho	iendayo
5. cha	ya	wa	za
6. wapili	mbili	wawili	muwili
7. yenye	chenye	zenye	kwenye
8. mwa	la	wa	vya
9. pakajaa	kukajaa	likajaa	ikajaa
10. hicho	hizo	hivyo	hiyo
11. ya	cha	za	wa
12. ilio	walio	ulio	kilicho
13. wa	ya	la	za
14. mji	kjji	jji	kji
15. Yule	wale	kile	vile

Tambua maumbo haya



a. _____

b. _____

c. _____

d. _____

Andika sentensi hizi kwa wingi.

a. Uta umewekwa ukutani _____

b. Kutibiwa kwangu kumenipinya. _____

Chagua msamiati halisi wa mahakama mabanoni

a. Aliyekamatwa na polisi hushtakiwa katika _____ (gereza, mahakama)

b. Jina jingine la gereza ni _____ (jela, mbaroni)

Andika maana ya majina haya.

a) Hakimu / jaji - _____

b) Mshtaki - _____

c) Mshtakiwa - _____

d) Shahidi - _____

e) Wakili - _____

Andika misemo tano na maana yake.

a. _____

b. _____

c. _____

d. _____

e. _____

Tumia kiulizi sahihi cha -pi?

1. Chakula __pi hakina chumvi?
2. Waliandika insha __pi?
3. Sungura _____ amezaa vitungule.
4. Vyoo _____ vimeoshwa.
5. Mjini _____ hakuna taa.

Jaza jedwali kwa kupachika "nomino" au "kitenzi" sahihi.

KITENZI	NOMINO
-----	kilimo
soma	-----

Kamilisha sentensi kwa tashbihi sahihi


- 1) Nguo hii ni nyeusi kama -----
- 2) . Kinywaji hiki ni chungu kama -----
- 3) Chafu kama -----
- 4) Safi kama -----
- 5) Mama Yule ni mvumilivu kama -----

Andika saa kwa maneno


a. 4 : 00 -----

b. 6 : 30 -----

c.



d.



Badili sentensi hizi ziwe katika usemi halisi au wa taarifa

Aliniuliza jina langu. -----

“ Juma, nenda shuleni haraka,” mama alimwambia. -----

Andika kitenzi kilichopigiwa mstari katika kauli ya kutendua.

Msusi **alianika** nguo.. -----

Waridi **alisafisha** hapa. -----

Tunga sentensi fupi fupi ukitumia misemo hii.

a. Kula chumvi nyingi -----

b. Kwenda haja kubwa -----

c. Kufa ganzi -----

Chagua jibu sahihi usanifishe sentensi

a. Mchanganyiko wa mahindi na maharagwe ni -----

b. Ndizi zilizopikwa ni -----

c. Maharagwe yaliyopikwa huitwa_____

d. Mchele uliopikwa kwa nyama na mapochopocho huitwa _____

e. Kaukau ni nini? _____

Badili vitenzi hivi katika kauli ya kutendwa.

Mfano: Nokoa ~~amelinunua~~ shamba.

Shamba ~~limenunuliwa~~ na nokoa.

Mwanafunzi ~~amebeba~~ vitabu. _____

Kamau ~~anachora~~ picha. _____

Kamilisha methali hizi kwa ufasaha.

Akili ni _____

Adhabu ya maiti ajuaye _____

Adui _____

Cha mwanafuu mkufuu ha _____, Cha mkufuu mwanafuu hu _____

Kamilisha sentensi kwa tamathali mwafaka

Runinga ilituletea _____ za kisiasa (kukurukakara, shelabela)

Barabara kuu ya Thika imenyoka _____ (pu,twa)

Tumia -o-ote kwa ufasaha kujaza nafasi

Watoto _____ wamekula.

Tunda _____ limeoza lote.

Tunga sentensi sahihi kwa kutumia -ote.

Teua jibu sahihi kujaza nafasi

Kiungo aina ya madini meupe kinachotumika kuongeza ladha katika chakula hutwaje? _____

Tunda jekundu la duara linalokatakatiwa katika kitoweo au wakati wa kukaanga ni _____

Soma hadithi hii kisha ujibu maswali.

Mcheshi ndilo jina lake. Mtoto wangu ninayempenda kama wasemavyo waswahili, sijui, chanda na pete, ulimi na mate au uta na upote.

Ni raha iliyoje kuwa na mtoto mwema, mpole, mcheshi, mwenye heshima na adabu zake. Mtoto ambaye akiitwa huitika “ Abel!” au “Naam!” Mtoto ambaye akitumwa hutumika na akikanywa hukanyika! Katika masomo ni mtiiFu na msikivu kweli kweli. Naam, huyo ndiye mtoto wa utotole si wa utovu kama walivyo wana wengine watovu wa maadili.

Kila mtu humpenda Mcheshi. Wakubwa kwa wadogo, wa kike kwa wa kiume, wazee kwa vijana. Wote kwake ni rafiki, jamaa, wapenzi na wasaidizi. Anasaidiana nao, anacheka nao, wanasaidiana popote wakati wowote. Hana ukabila wala ukoo. Kwanza ukabila ni nini? Upuzi mtupu! Ni nchi gani iliyombwa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kabila moja tu? Niambieni.

Hivyo ndivyo nilivyomwelekeza mwanangu Mcheshi. Anaamini kuwa binadamu wote ni ndugu zake na Taifa ni moja-letu. Analipenda Taifa lake na watu wake. Hakati miti, hachafui mito, maziwa, mabwawa, chemichemi wala hachezei maji ya mabomba. Huyatumia kwa uangalifu na kwa manufaa si kwa uharibifu. Je, wewe ni kama Mcheshi au ni kinyume chake? Anza leo. Tenda wema uwe mwema.

Maswali

- 1) Ukisema “wakubwa kwa wadogo” kama ilivyotumika katika hadithi hii utakuwa ukimaanisha nini? _____
- 2) Msemaji anampenda Mcheshi kutokana na nini? _____
- 3) Kwa nini watoto wengine wanaweza kukua wakiwa na tabia mbaya? _____
- 4) Tofautisha maana ya vitate hivi- kua na kuwa

- 5) Katika mazingira halisi ya Kiswahili ,mtu hafai kuitika vipi anapoitwa? (**naam!**, **abe !**, **eeh!**)
- 6) Kitendo cha kusaidiana mahali popote wakati wowote ni ishara ya nini? (uadui, uhasama, undugu)
- 7) Mtoto msikivu ni mtoto wa aina gani? _____
- 8) Taja sifa moja ya Mcheshi kutoka kwenye hadithi hii. _____
- 9) “ Hakati miti, hachafui mito, maziwa mabwawa...” Ni kidokezo kinachotupa wazo gani?

- 10) Toa kichwa mwafaka kwa habari hii _____